



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAASISI YA UONGOZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MAKAMU WA RAIS PHILIP ISDOR MPANGO KUFUNGUA KONGAMANO LA JUKWAA LA MAENDELEO ENDELEVU 2024

15 Aprili 2024, Dodoma: Mhe. Dkt. Philp Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mlezi wa Jukwaa la Maendeleo Endelevu anatarajiwa kufungua kongamano la nane la Jukwaa hilo leo, lenye dhima ya *“Kuhamasisha uwekezaji katika bustani za kijani kwa maendeleo endelevu Tanzania”*.

Kongamano hilo litahudhuriwa na viongozi kutoka kwenye maeneo mbalimbali nchini Tanzania – na wanaowakilisha sekta/taasisi mbalimbali ikiwemo sekta ya umma, sekta binafsi, taasisi za elimu ya juu na asasi za kiraia. Aidha, Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) atashiriki.

Washiriki wa kongamano watajadili masuala muhimu ya uwekezaji na usimamizi madhubuti wa bustani za kijani, ikiwemo masuala ya kisera, uzoefu kutoka nchi nyingine, ushirikiano na wadau, na fursa zilizopo. Vile vile, kongamano litajumuisha ziara katika moja ya bustani ya kijani inayosimamiwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Jukwaa la Maendeleo Endelevu ni moja ya programu kuu za Taasisi ya UONGOZI katika masuala ya maendeleo endelevu. Lengo lake ni kukuza uelewa wa masuala ya uchumi wa kijani na mchango wake katika maendeleo nchini Tanzania. Linawakilisha zana ya kimaendeleo ya kujenga miunganisho ya kisekta, kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kutunza mifumo ya ikolojia na mazingira. Tangu kuzinduliwa (2010), makongamano nane yamefanyika.

Ushiriki katika kongamano hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Suzana Aroko

Kaimu Meneja Mawasiliano